

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe: press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ikulu, Chamwino.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan leo tarehe 01 Mei, 2021 atakuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (*Mei Mosi*) ambayo Kitaifa yatafanyika katika uwanja wa CCM Kirumba Jijini Mwanza.

Sherehe za maadhimisho ya Mei Mosi zitaanza saa 3:00 asubuhi hii ambapo pamoja na kulihutubia Taifa, Mhe. Rais Samia atapokea maandamano ya wafanyakazi, risala ya wafanyakazi, atatoa zawadi kwa wafanyakazi bora na atatoa zawadi kwa washindi wa mashindano ya Mei Mosi.

Matangazo ya moja kwa moja (*mbashara*) ya sherehe hizo yatarushwa na vituo vya habari vya redio, televisheni na mitandao ikiwemo Youtube Channel ya Ikulu Mawasiliano na kurasa rasmi za Ikulu Mawasiliano za *Instagram, Twitter na Facebook*.

Gerson Msigwa
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU
01 Mei, 2021
Chamwino.